


# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



SHULE YA SEKONDARI KIGUGU,  
S.L.P 113,  
TUKUYU.

NAMBA YA SIMU: **0755 236 621**  
Kumb.Na.KSS/2248/KDI-2021/VOL XIV/.....

MWANAFUNZI:.....

S.L.P .....

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIGUGU WILAYA YA RUNGWE MWAKA 2021.

**1.0** Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari kigugu ipo umbali wa KM 5 (Tano) toka Makao makuu ya wilaya ya Rungwe.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021**, unatakiwa kuripoti shulenii tarehe 11/01/2021 saa moja kamili asubuhi mwisho wa kuripoti ni tarehe **17/01/2021**

### 2.0MAAGIZO YA SHULE

A	WAVULANA	A	WASICHANA
	(i) Suruali mbili (atashona mwenyewe) rangi ya kitambaa atapewa shulenii		(i) Sketi mbili (atashona mwenyewe) rangi ya kitambaa atapewa shulenii
	(ii) Viatu vyeusi jozi mbili		(ii) Viatu vyeusi jozi mbili
	(iii) Soksi nyeupe na ndefu jozi mbili		(iii) Soksi nyeupe jozi mbili
	(iv) Aje na sweta rangi ya damu ya mzee		(iv) Aje na sweta rangi ya damu ya mzee
	(v) Mashati mawili meupe mikono mifupi		(v) Mashati mawili meupe mikono mifupi
B	VIFAA VYA MICHEZO	B	VIFAA VYA MICHEZO
	(i) Bukta rangi ya kijani		(i) Bukta rangi ya njano
	(ii) Raba jozi moja		(ii) Raba jozi moja
	(iii) Fulana – t- shirt ya njano		(iii) Kigauni rangi ya njano
	(iv) Soksi nyeupe ndefu		(iv) Soksi nyeupe ndefu
C	VIFAA VYA KAZI	C	VIFAA VYA KAZI
	❖ Siku ya kufungua shule aje na ndoo ya plastiki lita 20 na Jembe likiwa na mpini		❖ Siku ya kufungua shule aje na ndoo ya lita 20, kwanja na “squizer” (ya kusukumia maji sakafuni)

### **3.0VIFAA VYA MASOMO**

Unatakiwa kuleta vifaa vya masomo kama ifuatavyo:-

- 1) Daftari za kutosha masomo yote tisa (9)
- 2) Kalamu za wino wa bluu au mweusi
- 3) Kalamu za risasi (penseli)
- 4) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)
- 5) Four figure (Mathematical table)
- 6) Kamusi ya kингereza
- 7) Faili moja (flatfile) kwa ajili ya kutunzia taarifa zake mbalimbali

### **4.0MAMBO MENGINE MUHIMU**

- (a) Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkoo wa Hospitali ya serikali.  
Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkoo wa Shule mara utakaporipoti shulenii.
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa shulenii.
- (d) Picha mbili (2) ndogo (passport size)

### **5.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

**5.1**Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi .Ukiwa hapa shulenii, unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:

1. Ni lazima kuwahi shulenii mapema asubuhi, kuhesabu namba, kuhudhuria masomo kila siku na kila kipindi na kuwepo shulenii kila siku na kila wakati.
2. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, kutii kengele, na kuwahi kila mahali utakapohitajika na kwa wakati.
3. Kuhudhuria shughuli zote za shule na zingine utakazopewa ukiwepo hapa shulenii.
4. Kuwaheshimu walimu, viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla. Pia uwe na ukarimu wa kumpokea yoyote anayefika shulenii mzigo alioubeba.
5. Ni lazima kuwaa sare za shule kila siku. Sare za shule ni pamoja na shati nyeupe kwa jinsia zote, suruali na sketi rangi ya damu ya mzee kwa siku za **Jumatatu, Jumanne** na **Jumatano**. Rangi ya kijani itavaliwa siku za **AlhamisinaIjumaa**. Mishono ya kubana (Modal) pamoja na sketi fupi haziruhusiwi.
6. Huruhusiwi kuwaa mavazi yaletayo aibu kama vile suruali/sketi za kubana, fupi mlegezo wala nguo yoyote, isiyo ya maadili ndani na nje ya shule. Adhabu kali itatolewa dhidi yako utakapogundulika.
7. Ni marufuku mwanafunzi kuwaa viatu vyenye kisigino kirefu, soli ndefu au pana wala kiatu kilichochongoka mbele, mkanda usio mweusi, mkanda wenye chuma, bajaji au mapambo mengine kama hereni, mkufu, ama bangili. Pia ni marufuku kuwa na nywele ndefu, kupaka kucha rangi, kupaka wanja, piko, kujichubua ama kunyoya kipara (zungu).

8. Unapaswa kutumia lugha ya kingereza katika mawasiliano na walimu pamoja na wanafunzi wenzako wakati wote utakapokuwa hapa shulenii.
9. Kukimbia mitihani na majaribio ya taaluma darasani ni kosa. Ukifanya hivyo utapewa adhabu kali ikiwemo kusimamishwa masomo.
10. Huruhusiwi kubaki darasani muda wa mstarini (Assembly), mdahalo (debate), kipindi cha dini kipindi cha michezo ama muda wa mstarini kipindi cha michezo ama muda wa clubs bila kibali cha mwalimu. Ukikutwa utapewa adhabu kali
11. Unatakiwa kuiheshimu tarehe ya kufunga na kufungua shule. Endapo utachelewa kufungua shule, utapewa adhabu kali ikiwemo ya kurudishwa nyumbani ama kusimamishwa masomo
12. Huruhusiwi kuingia ofisi ya walimu (Staffroom) ofisi za shule, maabara au nyumba za walimu kutumia/kuingia vyoo vya walimu bila ruhusa. Kufanya hivyo ni kosa la kinidhamu, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.
13. Unatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, wimbo wa taifa, wimbo wa shule, fedha ya nchi pamoja alama nyingine za taifa. Pia ni lazima kusimama kimya wimbo wa taifa unapoimbwa.
14. Huruhusiwi kufanya dharau, kiburi, uwongo, fitina, ubishi ama jambo lolote lililo kinyume na nidhamu ya shule dhidi ya mwalimu ama mfanyakazi asiye mwalimu.
15. Ni marufuku kumkimbia mwalimu au mfanyakazi asiyekuwa mwalimu, ni kosa kudanganya, kusema jina la uongo, kwa mwalimu, mtumishi ye yeyote ama kwenye mitihani, utapewa adhabu kali ukifanya hivyo.
16. Huruhusiwi kupiga au kupigana, kufanya vurugu ya aina yoyote, kupiga kelele zitakazovuruga utulivu wa darasa ama kutoka nje ya darasa muda wa vipindi. Ukifanya hivyo utasimamishwa masomo ama utafukuzwa shule kabisa.
17. Huruhusiwi / Ni marufuku kuruka dirishani, kuruka fensi/uzio /wigo ama kingo za maua. Pia huruhusiwi kutoka nje ya mipaka /maeneo ya shule bila kibali cha mwalimu. Ukikamatwa adhabu kali itatolewa dhidi yako ikiwemo ya kujenga upya wigo na kupanda maua mahali ulipopita.
18. Endapo utafanya uharibifu wowote ndani ya shule, utachukuliwa hatua kali ikiwemo kufukuzwa shule /kusimamishwa na kulipa gharama za uharibifu huo.
19. Ni wajibu wako kutunza usafi wa mwili na mazingira yote yanayokuzunguka popote ulipo. Kutupa taka ovyo na kuchafua kuta za madarasa ni kosa kubwa, hivyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yako. Pia huruhusiwi kulia chakula ama kunywea chai darasani.
20. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvalaa mojawapo ya sare ya shule (shati au suruali /sketi) kila siku ya Jumamosi utakapohitajika shulenii ama siku nyingine za sikuu utakapohitajika sweta la shule, soksi pamoja na viatu havitahesabika kama mojawapo ya sare hizo.
21. Hairuhusiwi mwanafunzi kukumbatiana na mwanafunzi wa jinsia tofauti au kusimama /kuongozana naye maeneo ya maficho ndani na nje ya shule. Ukgundulika utafukuzwa shule.
22. Ni marufuku kuvuta sigara, bangi wala kukutwa na kilevi cha aina yoyote ndani na nje ya shule. Kufanya hivyo ni kosa la jinai na itakupasa uvuliwe uanafunzi na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria
23. Mwanafunzi atatakiwa kusaidia kazi za jikoni (kazi ndogo ndogo) pale itakapobidi. Kwa mfano;
  - (a) Kusafisha vyombo vya chakula
  - (b) Kusafisha eneo la jiko
  - (c) Kuchota maji
  - (d) Kuokota kuni/kupasua kuni

**N.B:** Mwanafunzi yoyote haruhusiwi kupika chakula cha shule jikoni

24. Uwe mlinzi wa mali yako na mali ya shule pia

➤ **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha usimamishwe ama ufukuzwe shule;**

- (a) Wizi wa aina yoyote
- (b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku (90) bila taarifa (utoro)
- (c) Kupiga au kupigana
- (d) Uvutaji wa sigara, bangi, madawa ya kulevyaa ma ulevi wa aina yoyote
- (e) Ubakaji
- (f) Kupata au kusababisha mimba
- (g) Kuharibu kwa makusudi mali za shule
- (h) Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa taifa
- (i) Kuoa au kuolewa
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kugoma, kuchoea kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu  
(kugoma ama kuhamasisha mgomo)
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (m) Kuwa/kumiliki simu ya mkononi
- (n) Kudharau walimu, wafanyakazi wasio walimu ama viongozi
- (o) Kutoa lugha ya matusi/lugha chafu
- (p) Kutembelea majumba ya starehe, nyumba za kulala wageni (guest house) n.k
- (q) Kosa lolote la jinai
- (r) Makosa mengine yafananayo na hayo hapo juu.

**6.0**Tafadhali soma maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

P O BOX 113  
**TUKUYU-MBEYA**  
**'KARIBU SANA KATIKA SHULE HII'**

.....  
**ZAKARIA J. MWAKATOBE**

**MKUU WA SHULE**

# **WIAZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

## **SHULE YA SEKONDARI KIGUGU**

### **FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

#### **SEHEMU A:**

1. Jina la mwanafunzi:.....
  2. Mwaka wa kuzaliwa: .....
  3. Jina la mzazi/mlezi: .....
  4. Uhusiano: ..... kazi yake: .....
  5. Anuani ya mzazi/mlezi : .....
  6. Mahali anapoishi mwanafunzi: .....
- Umbali kuja shulenii ni km .....
- Majina ya ndugu/ mlezi mwininge wa karibu:-

S/N	JINA	UHUSIANO	NAMBA YA SIMU
i)			
ii)			
iii)			
iv)			

**7. MENGINEYO:-** .....(kama mgonjwa, yatima, mlemavu).

#### **SEHEMU B:**

#### **TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIGUGU.**

Mimi ..... nimezisoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na kwamba niko tayari/siko tayari kuzifuata.

Sahihi ya mwanafunzi: ..... Tarehe : .....

#### **TUKUYU-MREYA**

#### **SEHEMU C:**

#### **TAMKO/AHADI YA MZAZI/ MLEZI:-**

Mimi ..... Ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi .....

Nitatekeleza/sitatekeleza maagizo na mahitaji yote muhimu ya shule kama (nilivyo/nitakavyo)elekezwa na kwamba niko tayari/siko tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu ili kuinua taaluma na nidhamu yake.

Sahihi ya mzazi/mlezi ..... Tarehe : .....

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

To the medical Officer,

From:.....

.....  
.....

Date: .....

Re: .....

Please Examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time secondary schools studies that may also include military training the Examination should include the following categories (1, iv) each category or sub-category which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnant (category IV) will also render a girl candidate ineligible for the cause.

- I. (a) Eye sight
- (b) Hearing
- (c) Speech
- (d) Limbs
- (e) General disease
- (f) Leprosy
- (g) Epilepsy

Other serious disease .....

Pregnancy .....

**PART B: MEDICAL OFFICER.**

(To be completed by a Government Officer)

I have Examined the above named and consider that he/she is physically fit for a full time secondary school studies.

- (a) Eye – sight
- (b) Hearing
- (c) Speech
- (d) General disease
- (e) Leprosy
- (g) Epilepsy

II. Neuroses .....

III. Other serious diseases.....

IV. Pregnancy .....

Date: .....

Signature: .....

Station: .....

Date: .....